# Matumizi ya Ukweli Kinzani Kama Mtindo katika Nyimbo za Les Wanyika na Simba Wanyika

Job Nyongesa Juma

*Department of Languages, Africa Nazarene University*
*E-mail: jayjuma52@yahoo.com ; ORCID: https://orcid.org/0009-0000-1159-3890*

APA Citation: Juma, J. N. (2025). Matumizi ya Ukweli Kinzani kama Mtindo katika Nyimbo za Les Wanyika na Simba Wanyika. *Ngano: The Journal of Eastern African Oral Literature*, 3, 117-123.

**Ikisiri**

*Makala hii ililenga kutambulisha aina mbalimbali ya ukweli kinzani kama mtindo wa kazi ya kifasihi. Utafiti wa maktabani na mtandaoni ulifanywa ili kuweza kutambulisha nyimbo za watribu wa rumba wa bendi ya Wanyika. Nadharia ya uhalisia ilitumika katika utafiti huu. Mihili ya nadharia hii ilitufaa katika uchambuzi wa data. Data zilipatikana kutoka kwa nyimbo za bendi hii ya Wanyika. Ukweli kinzani kama mtindo ilitumika ili kuafiki ujumbe wa bendi hii. Ilibainika wazi kuwa mtindo na maudhui ni kama uti na mgongo. Aina mbalimbali za ukweli kinzani zilijitokeza katika uchambuzi wa data. Ukweli kinzani baina ya mtu na jamii ulishamiri sana katika mifano kwa vile matarajio ya jamii na mienendo za mtu hukinzana kila mara. Kuna ukinzani wa mtu binafsi ambapo binadamu mwenyewe anatenda kinyume na matarajio yake. Mbinu hii ni mbinu ambayo inatambulisha kejeli na mbinu zingine kama kinaya katika matumizi yake. Ni vyema mtunzi wa kazi ya sanaa ya fasihi hususani nyimbo atilie maanani dhana au suala la mtindo katika utunzi wake. Kundi la Wanyika lilijenga muumano wa kutolea mfano kati ya mtindo na maudhui.*

**Maneno Muhimu:** *Unafiki, Mtindo, Ukwelikinzani*

## UTANGULIZI

Binadamu hupata burudani kupitia kwa njia mbalimbali. Nyimbo ni moja wapo ya njia ambazo binadamu hupata nafasi ya kujiburudisha. Historia ya nyimbo kama moja wapo ya kipera cha fasihi inaambatana na uwepo wa binadamu. Huwezi tenganisha nyimbo na binadamu. Utanzu hii hudhihirisha kuwa utamaduni wa jamii ni muziki. Muziki umekuwa chombo ambacho kimewavutia wanadamu. Jambo hili limewafanya watu wa matabaka mbalimbali wakiwemo wanafalsafa na watu wa kawaida kujaribu kuelewa muziki lakini hakuna fasili ambayo imeweza kueleza muziki ni nini hasa: Uasili wake haujulikani, kama anavyodai Schumann (1994) kuwa: "Sayansi hutumia hisibati na umantiki, ushairi nao hutumia maneno teule. Muziki ni yatima ambaye babake na mamake hawajulikani kamwe. Hata hivyo, ni huu utata wa uasili wake ambao umefanya muziki uonekane kuwa kitu bora zaidi katika jamii" (Tafsiii yangu). Nyimbo za makundi ya Wanyika zilikuwa moto wa kuotea mbali. Vibao vyao vinaporindima na kupasua mawimbi ya burudani, vizazi vyote hutii na hata wale waliokosa kuwepo vibao hivi vikiwika. Wafuasi hawa huwa wengi wa kumbukumbu za maswala ya kijadi na mambo ya nyakati za nyuma. Ni nyimbo zilizotungwa kistadi na kusheheni mashairi na ushauri sufufu. Wanzilishi wa bendi hii walikuwa: William Kinyonga, Geroge Kinyonga na Wilson Kinyonga wazawa wa Rwanda lakini wakachipukia Tanzania na Kenya. Simba Wanyika ilikuwa bendi nchini Kenya iliyoundwa mwaka wa 1971 na ndugu kutoka Tanzania, Wilson Kinyonga na George Kinyonga. Bendi hii ilivunjika mwaka wa 1994. Simba Wanyika na bendi zingine mbili zilizotoka kwayo, Les Wanyika na Super

Wanyika Stars, zilikuwa bendi mashuhuri sana nchini Kenya. Muziki wao uliotokana na sauti ya gitaa, ikiongozwa na mpiga gitaa wa Soukous, Dr Nico, ikichanganywa na maneno matamu ya muziki wa rumba na kuimbwa kwa Kiswahili. Simba wa nyika tafsiri yake kwa Kiingereza ni "Lions of the Savannah". Vibao vya kundi hili ni kama "Sina Makosa", "Jessica", "Barua Yako", "Paulina", "Afro", "Kwanza Jiulize", "Tafuta Wako", "Kajitu liza Kasuku", "Nimaru", "Wazazi", "Mbaya Wako Rafiki Yako", "Pamela", "Shirika la Mapenzi", "Ufukara sio Kilema", "Amigo", "Safari ya Samburu", "Nisaidie Baba", "Ni Lipi la Ajabu", "Heshimuni Wazazi", "Esther Nikumbuke", "Sioni wala Sisikii", "Penzi Halina Siri", "Mke wa Kwanza", "Nimebaki Upweke", "Safari Sio Kifo", "Mzazi Wangu Mama", "Mama Watoto", "Dunia Kigeugeu","Usia wa Baba", na vinginevyo. Kundi hili lilifanya kazi na mwimbaji hodari John Ngereza na mpiga ala Omar Shabani.

Swali ambalo kila mja hujiuliza ni nini kilipelekea nyimbo za ndugu hawa kutawala nchi za Afrika Mashariki na hata kuvuka mipaka ya bara zingine? Majibu ni mengi kwa vile muziki huambatanishwa na vipengele mbalimbali. Makala haya yamelenga kushughulikia matumizi ya ukweli kinzani katika uwasilishaji wa nyimbo hizi. Mbinu hii ilifaa utunzi huu wa Wanyika? Ukweli kinzani hujitokeza katika mifumo ipi? Haya ndiyo baadhi ya maswali ambayo utafiti huu unajaribu kushughulikia. Mtindo ndiyo hutambulisha mwimbaji na ukweli kinzani ndiyo mtindo unaotambulisha waimbaji wa kundi la Wanyika.

## MBINU, MALENGO NA SABABU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa maktabani na katika mtandao. Vitabu vilisomwa na muziki wa kikundi cha Wanyika ulisikizwa na data muhimu kuweza kunukuliwa. Nyimbo mbalimbali zilisikizwa ila ni zile tu zilizoakisi malengo ya utafiti huu ndizo zilinukuliwa na kutumika katika utafiti huu. Mbinu ya usaili ilitumika katika kuelezea matokeo ya utafiti huu.

Utafiti huu una malengo yafuatayo:

- Makala haya yanalenga kudhihirisha ushirikiano uliopo baina ya mtindo wa ukweli kinzani na maudhui katika kufanikisha nyimbo.
- Kutambua aina mbalimbali za ukweli kinzani katika nyimba za Simba na Less Wanyika.

Utafiti huu ulikuwa muhali kufanyika kwa sababu zifuatazo:

- Uwepo wa wapenzi wa mziki huu kwa wingi katika jamii ya Afrika Mashariki na hata katika dunia nzima. Pengine sababu ya umaarufu wao inaweza kuwa jambo la kuigwa na wanamziki wengine.
- Kurahisisha uwelewaji wa nyimbo hizi kwa jamii ya sasa.

## YALIOANDIKWA KUHUSU UKWELI KINZANI

Hii ni mbinu ambayo huonekana ikijipinga kijuujuu ingawa inapochunguzwa kwa makini inadhihirisha ukweli fulani (Corbett, 1971). Akijalizia maelezo ya Corbett, Wamitila (2008) anaeleza kuwa katika kuchunguza kweli kinzani, mambo mawili ya kimsingi yanahitajika. Kwanza, kutambua maana ya kijuujuu ambayo inaonyesha huu ukinzani na pili, maana ya ndani na ambayo ndiyo haswa aliyoikusudia mwandishi kumpokeza msomaji wake. Hii maana ya pili ndiyo inahitajika msomaji aitambue licha ya kusaidia katika kukuza ukinzani huo uliopo.

Balidick (1999) anaeleza kwamba, kweli kinzani ni kauli au matamshi ambayo kwa njia ya kushangaza mno na kuzua mgongano na kujikinza kiasi cha kutuchochea kuwaza ya muktadha

mwingine ambamo hali iliyoelezwa inaweza kuwa kweli. Mfano wa kweli kinzani ni kauli ‘mtoto ndiye baba wa mwanamume”. Katika muktadha mpana dhana kweli kinzani huweza kuelezea mtu au hali ambayo ina sifa wazi za ukinzani. Ufafanuzi huu umeonyesha kuwa kweli kinzani ni kauli ambayo ina mawazo mawili kinzani ambayo hali kuwa isiyowezekana kamwe au isiyo ya kawaida, ingawa huenda ikawa ni kweli. Ni kweli iliyokama uongo, neno linaloonekana kama kwamba ni la kinyume kumbe ni sahihi. Pia mtu, kitu au hali ambayo ina sifa mbili ambazo ni kinyume na kwa hivyo kuonekana kuwa ajabu. Methali za paradoksia ni mfano wa maelezo haya; methali ambazo hukinzana wakati wa kuzifasiri kwa msingi wa kimaantiki. Kimsingi kinachosemwa kinaonekana kukinzana kijuujuu lakini kinapochunguzwa kwa makini kinaonyesha ukweli fulani. Mfano wa methali za kweli kinzani ni pamoja na:

*Kufa kwa wengi ni harusi*
*Kupotea njia ndiko kujua njia*
*Mkono usioweza kuukata ubusu*
*Adui mpende*
*Ndugu wakigombana chukua jembe ukalime, wakipatana chukua kapu ukavune.*
*Wagombanao ndio wapatanao.*
*Ukupigao ndio ukufunzao.*
*Kuinamako ndiko kuinukako.*
*Mwenye kelele hana neno.*
*Kimya kingi kina mshindo mkubwa.*

## NADHARIA YA UHALISIA

Msingi wa uhalisia unadhaniwa kuwa ulitokana na suala la mwigo (mimesis) lililodokezwa na Aristotle katika Poetics ya 335 KK (Snircova 2015: 8). Aristotle alieleza kuwa silika ya binadamu ilimfanya aige vitu vilivyoko karibu naye na hatimaye kuanza kujitungia sanaa ili kuwakilisha kile alichokiona kama vile tanzia na futuhi. Binadamu aliweza kuiga vitu kwa namna mbalimbali: jinsi vilivyo, jinsi vinavyosemwa vipo na jinsi vinavyopaswa vionekane (Snircova 2015 keshatajwa). Nadharia ya uhalisia inarejelea mwigo ambapo binadamu huiga vitu jinsi vilivyo na hatimaye kubuni kazi ya sanaa husika. Ubunaji huu unamtaka mtunzi kutumia njia anuwai za kiufundi katika uwakilishaji wa kazi yake. Anapofanya hivyo basi anarejelea jamii na mazingira husika. Hata hivyo, wataalamu wengine wamesisitiza kuwa matumizi kamili ya nadharia ya uhalisia katika fasihi yalianza kuonekana katika kazi ya Erich Auerbach ya 1948 iliyojulikana kama Mimesis (Ruan 1986: 1).

Wanafasihi waliochunguza historia ya uhalisia kama vile Vernon Louis Parrington huidhukuru kama nadharia iliyochipuka katika miaka ya 1870 na 1880 (Pizer 1995: 103). Uhalisia wa kifasihi ulianza kudhihirika katika karne ya 19 na mwanzo wa karne ya 20 (Abrams 1988: 153; Marques Pedro 2009: 3; Taghizadeh 2014: 1628). Matumizi yake katika fasihi yalitokana na wasanii kama vile Honoré de Balzac, George Eliot, William Dean Howells (McGowan 1980: 171; Abrams 1988: 154), na Ambrose Bierce, Henry James, Cesare Pavese, Primo Levi, Stendhal, Gustave Flaubert na Emile Zola (Snircova 2015: 10). Kuchipuka kwa tapo la uhalisia kulisababishwa na hali ya kimuktadha na kitamaduni ya huko Ulaya katika karne ya 19 hasa katika nchi za Ufaransa na Uingereza. Katika nchi hizi, hali halisi ya ulimwengu ilionekana ikihusisha masuala kama vile maendeleo ya viwanda, sayansi na nguvu za watu wa tabaka la kati (Snircova keshatajwa). Hali hizi zilichangia uundaji wa mifumo mipya ya imani na maadili. Hivyo basi, waandishi weniI pamoja na hadhira wakaanza kuona mambo ya mifumo hiyo mipya jinsi yalivyokuwa kiuhalisia katika mazingira yao na sio jinsi walivyoambiwa.

Riwaya halisia ya kwanza ya Kiswahili imechukuliwa kuwa Utubora Mkulima (1968) iliyotungwa na Shaaban Robert (Mbatiah 2001: 71). Kufikia miaka ya 1960 na kuendelea, riwaya nyingi zikatungwa kwa msingi wa uhalisia kama vile Kurwa na Doto (1960) ya Muhammed Saleh Farsy (Rettová 2016: 20-21). Watunzi wengi wa riwaya za Kiswahili walianza kutumia uhalisia mamboleo katika karne ya ishirini na moja kwa sababu ya mvuto wa ubunifu huku riwaya hizi zikitarajiwa kutoa maelezo na ushawishi, masuala ya kisiasa na kiuchumi, falsafa ya kuchanganya uhalisia na uhalisia wa kimaajabu, na upokezi wa kazi hizi.

## UKWELI KINZANI KATIKA NYIMBO

Bendi hii ilicharaza wimbo maarufu kwa jina *Shilingi Yaua tena Maua*. Less Wanyika wanasisitiza umuhimu wa shillingi katika dunia. Wanasema kuwa hata ukiwa vipi bila shillingi wewe ni bure. Ujumbe wao unachembe za kukinzana wanaposema kuwa hata ukiwa na sura nzuri vipi bila shillingi huwezi pendwa. Hali hiyo ni kinyume na matarajio. Tunatarajia mtu wa sura nzuri ependwe lakini ni kinyume cha matarajio. Waimbaji hawa wanazidisha matumizi ya mbinu hii kwa kusema kuwa shillingi ni maua tena inua. Hali hii ni ya ajabu kwa kuwa shillingi inakufanya uibe na tena wakati uo huo inakufanya kuwa afisa. Ukiwa mzee na una pesa utapendwa na wasichana na kijana abaki papo hapo. Pesa ndio ufunguo wa mapenzi katika jamii ya sasa. Katika wimbo huu watunzi wanatoa mfano wa mzee wa miaka hamsini ambaye anaandamwa na wasichana kwa sababu ya shillingi. Shillingi isipokuwa katikati ya penzi mambo huaribika. Kwa hivyo, shillingi hii isipokuwepo katika penzi inaua penzi miongoni mwa wapenzi. Wanasema kuwa ukiwa na mpenzi wako na una uneni mtupu unaweza ishia kupoteza usiporusha shillingi mezani. Ukimuona mwanamke anapita vile na vile wewe unahitaji kutoa shillingi na utakukubaliwa haraka. Maneno matupuu hata yawe mazuri vipi hayavutii wanawake katika Afrika.

Kibao cha *Lift Niliokupa* inadhihirisha tabia za binadamu za kukosa shukurani. Wanyika wanasikitika kwa unafiki wa mama jirani nyumbani Kariakor. Mama anaeneza uvumi kuwa alimbeba garini ili kiwe kishawishi cha kumfanya mpenzi wake. Jambo la ajabu ni kuwa mwanamke huyu ndiye aliomba kusaidiwa. Waimbaji hawa wanatambulisha jambo lingine la ajabu kuwa huyu mwanamke hasemi mambo mengine ya nambari ya simu aliompa bwana huyu. Hili ni baada ya kuarifu mke wa jirani yake kuwa alimtaka kimapenzi na ilhali bwana huyu alifanya jambo la busara na heshima kumbeba. Mwanamke huyu amejitia hamnazo ni kama hakuwa na haja na bwana huyu aliyemuomba nafasi ya kubebwa. Mwanamke huyu ni mnafiki, lengo lake ni kuharibia bwana huyu sifa mtaani Kariokor.

Tabia hii ya unafiki inaendelezwa katika wimbo *Matamshi yako rafiki*. Katika wimbo huu wananyika wanatambulisha kisa ambapo jamaa mmoja hakupendezwa na tabia za mpenzi wake. Jamaa huyu haamini kwa kile ambacho alifanyiwa na mpinziwe. Lakini cha ajabu anasema kuwa yeye ni mpita njia. Anashauri mpenzi huyu asiwe na mashaka kwa sababu yeye anasonga mbele. Ni kinyume cha matarajio kwa yule aliyekosewa kutoa msamaha na kuahidi kuwa ataendelea na maisha na ilhali wakati uo huo ansikitika kwa kutendewa unyama. Hali hii inazidishwa kwa mwimbaji huyu kumshauri mpenziwe abaki na mpenzi mwingine ambaye wamezoeana. Wimbo *Safari ya Samburu* unakinzana na wimbo wa *Matamshi yako rafiki*. Katika wimbo huu waimbaji hawa wanadhihirisha kuwa ni muhimu kuwa na marafiki wakati uo huo anapotambulisha marafiki kama wanafiki katika wimbo. Anashukuru Bi. Josephina kwa kumuonyesha imani na mapenzi. Pia anawashukuru ndugu maina na Omollo kwa kumwonyesha mapenzi ya dhati. Anahidi kuonana nao tena.

Tabia ya wanaume ya kujifanya kuwa kwa hiari wametengana na bwana zao milele, kumbe kwa undani bado wanahisia za mapenzi nao zinajitokeza katika wimbo *Esther*. Waimbaji wanarejelea kisa cha bwana aliyempenda Esther hata baada ya kuambiwa Esther ana mchumba mwingine. Vilevile, wanakariri kuwa bwana huyu anajuwa kuwa kuna mwisho wa kila kitu lakini yeye haoni ikiwa kuna mwisho wa penzi lake na Esther anasema kuwa:

*Mawazo yangu yako kwko*
*Imani yangu iko kwako*
*Furaha yangu iko kwako*
*Mapenzi yangu yako kwako*
*Fikiri tena mabo hayo*

Mwisho anatambua Esther kama mpenzi wake na anamuomba kufikiria kuhusu huba lake. Wimbo huu unadhihirisha kuwa si rahisi kihisia wapenzi kutengana. Esther hata baada ya kupata mpenzi mwingine anaandamwa na mpenzi wake wa awali. Mpenzi huyu anamatarajio kuwa Esther atakuja kumkumbuka siku moja. Wimbo *Mambo* unatambulisha hali hii kinzani. Bwana anatambua kuwa mke wake hamtaki lakini anavumilia tu. Mwishowe anampata na picha ambazo zinazua mambo mengi katika ndoa yake. Bwana huyu anakiri kuwa alikuwa anajua kuwa mke huyu lengo lake lilikuwa kusambaratisha ndoa yao. Kupitia nyimbo hizi kundi hili la Less Wanyika linaonya wanaume dhidi ya kuvumilia katika penzi ambalo ni katili. Mwisho wa penzi hili huwa ni mikasa na vioja.Ukweli kinzani huu ni wa upungufu wa binadamu kimawazo na fikira. *Dunia Kigeugeu* ni wimbo mwingine ambao mwimbaji anatambua kuwa ameachwa lakini ana imani ya mke kurudi. Ameachwa kwa sababu ya umasikini. Anaamini kuwa siku moja atakuwa tajiri kama wengine. Anakumbuka kuwa waliahidiana kuishi pamoja hadi watenganishwe na kifo. Anasema mpenzi wake hakuwa hivyo, dunia ni kigeugeu kwake.

Wimbo *Sina Makosa* anatumbulisha hulka hii ya wanaume kuwaacha wake wao na kulumbania wake wengine katika mikahawa. Waimbaji hawa wanarejelea kisa cha jamaa mmoja ambaye anataka kumua mwenzake kwa sababu ya hawara. Jamaa huyu anashangaa, hasira na chuki ni za nini kati yao? Ilhali hakuna yeyote ambaye anamiliki mke yule na zaidi kila mmoja ana wake nyumbani. Bwana anaishia kusema kuwa hana kosa lolote kumpenda yule hawara.

*Hasira ni za nini bwana*
*Wataka kunuia bure, baba*
*Yule si wako name si wangu*
*Chuki gani kati yangu nawe*
*elelile Lelelilo oh Mama*
*Hasira za nini wee bwana*
*Hasira za nini wee bwana*
*Wataka kuniua bure baba*
*Wataka kuniua bure baba*
*Kwako hayuko*
*Kwangu hayuko*
*Chuki ya nini kati yangu*
*Mimi na wewe*
*Chuki ya nini kati yangu*
*Mimi na wewe*

Wanyika katika wimbo huu wanaonya tabia ya wanaume kuuana kwa sababu ya hawara ilhali wana wake wao nyumbani. Anatambulisha tabia ya ubinafsi na uchoyo wa mapenzi kwa wanaume. Mwanamume hataki kumiliki hawara na mwanaumume mwingine.

Bendi hii ilicharaza kibao kingine cha kumshauri mwanaume ambaye anafanya kazi na hawezi kushughulikia familia yake kwa sababu gharama zake hazina maana. Wanamwambia kuwa thamani ya mke ni kumlisha vizuri na kumvalisha nguo nzuri. Watoto awape elimu nzuri. Majirani walimkanya awaheshimu watoto na mke wako. Heshimu baba na mama nyumbani. Lakini akaona majirani na marafiki kuwa wabaya na vilevile yeye bingwa wa maisha. Akakosa kuwa na habari na mke wake kisha akamuacha sasa ubingwa wake uko wapi? Leo mambo yamemharibikia amigo.

*Dunai haina wema* ni kibao kingine ambacho kina kauli za ukinzani. Kibao hiki kina kinzana na kibao cha kundi hili cha Maisha ni mapambano. Katika kibao cha Dunia haina wema waimbaji hawa wanakariri umuhimu wa mja kutenda wema na kwenda zake. Wanaamini kuwa mja ndiye humlipa binadamu. Lakini katika kibao cha *Maisha ni mapambano* wanamziki hawa wanatoa nasaha kuwa maisha ni mapambano na ni vyema mja kufanya kazi kwa bidii kwani Mungu atawabariki. Wimbo wa *Dunia haina wema* una dhihirisha wazi kuwa huna la kusubiri katika dunia lakini binadamu anahamasishwa na kushauriwa kuvumilia. Huu ni ukinzani wa wimbo dhidi ya wimbo mwingine.

Kibao cha Sioni wala sisikii kinatambulisha ukweli kinzani. Mpenzi anashangaa kuwa ana macho na masikio lakini hasikii. Anatamani kujuwa penye mpenzi wake yupo. Alimuaga kuwa anaenda mapumziko Mombasa ya mwezi mmoja mbayo imekuwa ni mwaka mmoja sasa. Mke hajamueleza mahali alipo na hajui nani amemsusua au ni shida ipi imempata. Mpenzi hajanena chochote kwa muda wa mwaka mmoja. Bwana huyu bado anamsubiri baada ya kumtafuta sehemu nyingi za taifa kama Voi. Mombasa, Kitui, Eldoret na Busia. Baada ya kumkosa anaamua kurudi Nairobi tena kumsaka na ilhali alimuaga kuwa anaenda Mombasa. Akazidhisha kuenda Unguja, Pemba, Kampala Mbarara. Arusha, Tanga nab ado anataka kurudi Nairobi na hasikii chochote. Anaahidi kutembelea Nyeri, Awendo, Muranga, Nanyuki, Bungoma, Taveta na Undanyi. Mpenzi huyu anafanya hivi na ilhali anajua vizuri kuwa Mombasa kwenda ni rahisi lakini kurudi ni ngumu. Anazidi kuteseka kumtafuta mpenzi wake na ilhali hamshughulikii yeye kwa kumuambia alipo. Kibao hiki kinaonyehsa jinsi binadamu hupata ugumu wa kufanya uamuzi wa kuachana na mpenzi anayemlaghai kimapenzi. Bwana huyu haamini kuwa ameachwa hata baada ya kusahaulika kwa zaidi ya mwaka mmoja na matumaini ya kupatana na mpenzi wake. Kwa mfano anamwambia fanya hima urudi yeye hajui atampata wapi Sherry ambaye ndiye mpenzi wake.

## HITIMISHO

Makala haya yamelenga kubainisha matumizi ya ukweli kinzani katika nyimbo za Less Wanyika. Nyimbo ainati zmetumika kutambulisha mbinu hii. Ni wazi kuwa, waimbaji wa kikundi hiki waliafiki malengo yao kwa kutumia mbinu hii. Aina mbalimbali za ukweli kinzani zimedhihirika katika nyimbo hizi. Mtindo huu uliwezesha bendi hii kuweza kuwasilisha ujumbe na kufurahisha hadhira yake kwa burudani la mziki.

## MAREJELEO

Abrams, M. H. (1988). *A Glossary of Literary Terms* (5th Edition). New York: Holt, Rinehart & Winston.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks.

McGowan, J. P. (1980). The Turn of George Eliot's Realism. *Nineteenth-Century Fiction, 35*(2), 171-192.

Rettová, A. (2016). Writing in the Swing? Neo-realism in Post-experimental Swahili Fiction. *Research in African Literatures, 47*(3), 15-31.

Ruan, W. (1986). *Arnold Bennett. A Study in Realism*. PhD, University of Edinburgh.

Snircova, S. (2015). *Realism, Modernism, Postmodernism. Five Modern Literary Texts in Context*. Košice: Univerzita Pavla Jozefa Šafárika v Košiciach.

Taghizadeh, A. (2014). A Theory of Literary Realism. *Theory and Practice in Language Studies, 4*(8), 1628- 1635.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.